

HALMASHAURI YA WILAYA YA SUMBAWANGA

SHULE YA SEKONDARI ILEMBA,

S.LP 783,

SUMBAWANGA.

TAR.....

JINA LAMWANAFUNZI.....

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ILEMBA MWAKA

1. Nina furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha katika shule hii. Shule ya sekondari ilemba inapatikana wilaya ya sumbawanga vijijini mkoani rukwa. Muhula wa kuaza masomo unaaza Tar. unatakiwa kuripoti shuleni mapema kuazia Tarehe hiyo na mwisho wa kuripoti ni Tar.

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. SARE ZA SHULE

A) WAVULANA

Sare za shule hii ni;

1. suruali 2 ambapo 1 ni ya rangi nyeusi na 1 ni rangi ya bluu bahari zote ni kwa mshono wa malinda na turn up (mkunjo miguuni). *Suruali modo hazikubaliki*
2. Mashati mawili meupe mikono mifupi.
3. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba pea mbili na soks nyeusi pea nne.

B) WASICHANA

1. Sketi 1 nyeusi 1 ya bluu bahari ndefu usawa wa kugusa enka ya mguu, malinda yawe ya kawaida yasiwe membamba wala ya box
2. Mashati 2 meupe mikono mifupi
3. Viatu vya ngozi vya kufunga na kamba pea mbili na soksi nyeupe pea nne
4. Rangi ya hijabu ifanane na rangi ya sare za shule (kwa wasichana wa dini ya kiisilamu)

Kila mwanafunzi awe na walau pea 1 ya nguo na raba za michezo (sports gear).

2. VIFAA VYA USAFI

Kila mwanafuzi awe na vifaa vya usafi wa mazingira kama vile mifagio, ndoo, jembe

3. MAHITAJI YA HOSTEL

Kwa wanafunzi wa hostel inatakiwa kuja na michango ifuatayo:

- i. Mahindi gunia 2 kwa mwaka
- ii. Maharage debe 3 kwa mwaka
- iii. mpunga debe 3 kwa mwaka
- iv. Fedha Tsh.60,000/= kwa mwaka (kwajili ya mpishi na mahitaji mengine jikoni)
- v. Godoro 1 dogo la futi 2na nusu
- vi. mashuka ma wili rangi ya pinki
- vii. Vyombo vya chakula; kikombe, sahani, bakuli na kijiko
- viii. Ndoo 2 za lita 10 kwajili ya matumizi yake.

Kwakuwa shule inaendeshwa kwa mjibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na ina zingatia miongozo yote inayo tolewa na wizara yenye dhamana hapa nchini, Mwanafunzi hata pokelewa endapo haja timiza maagizo yaliyo tolewa hapo juu. Kila mwanafunzi ni lazima afuate sheria za shule wakati wote awapo ndani na nje ya shule.

KARIBU SANA ILEMBA SEKONDARI.



MKUU WA SHULE
ILEMBA SEKONDARI
S.A.P 783
SUMBAWANGA